

7 JUNI, 2013

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Arobaini na Tano - Tarehe 7 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

### NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:-

Taarifa za Mwaka za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mwaka 2008/2009, 2009/2010 na 2010/2011 (*The Annual Report of the Commission for Human Rights and Good Governance for the Years 2008/2009; 2009/2010 and 2010/2011*).

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona alivyosema Waziri ni kwamba ilikosewa, sio taarifa za mwaka za hesabu zilizokaguliwa; ni taarifa za Tume za mwaka. Kwa hiyo, hesabu zilizokaguliwa imeondolewa hapo.

7 JUNI, 2013

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 358

### Kukamilisha Ujenzi wa Zahanati Nchini

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Ujenzi wa Zahanati kwa kila kijiji nchini ulianza kwa hamasa kubwa, na wananchi wakajenga majengo kufikia mtambaa panya lakini Serikali imeshindwa kumalizia majengo hayo kutokana na kutenga kiasi kidogo mno cha pesa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa Zahanati hizo?
- (b) Je, Serikali halioni kuwa inawakatisha tamaa wananchi ambao wamekuwa wakijitolea kushiriki mpango huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (TAMISEMI)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ujenzi wa Zahanati kila kijiji unafanyika kwa kushirikisha nguvu za wananchi kuititia Mpango wa fursa na vikwazo katika maendeleo.

Aidha Serikali huchangia nguvu kidogo ili kuwezesha ujenzi huo kukamilika kwa wakati. Hadi sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kushirikisha nguvu za wananchi imekamilisha ujenzi wa Zahanati 15 na nyumba za watumishi 17. (*Makofi*)

Vilevile ujenzi wa Zahanati 23 upo katika hatua mbalimbali za umaliziaji. Kwanza kabisa, nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa maeneo hayo kwa kazi kubwa ya ujenzi wa Zahanati hizo kwa lengo la kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha ujenzi wa Zahanati hizo 23 ambazo zimeanzishwa kwa nguvu za wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeidhinishiwa katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kiasi cha shilingi milioni 204/- kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kiasi cha shilingi milioni 191.2/- zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu za watumishi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama maelezo yaliyotolewa katika sehemu (a) hapo juu, Serikali imetenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Zahanati ambao ulianza kwa nguvu za wananchi. Hivyo azma ya Serikali ni kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati ili kutokuwakatisha tama wananchi ambao wanafanya kazi kubwa kwa maendeleo ya sekta hii. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ile inayoibuliwa na wananchi kwa kadiri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu. (*Makofii*)

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Wakati mpango huu wa kuboresha afya vijijini ulipoanza Serikali ilikuwa inatenga karibu bilioni 20/- kila mwaka.

Lakini imeendelea kupunguza fedha hizo mpaka kufikia mpaka bilioni 3/- mwaka jana. Sasa sijui Serikali imeridhika na hali hiyo kwa sababu wakati huu ndiyo wakati ambapo watu ndiyo wamekazana kujitolea kujenga zahanati. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze.

Je, Serikali kwanini inapunguza pesa hizo na kutenga fedha kidogo sana? (*Makofii*)

Lakini la pili ni kwamba fedha ambayo imetamkwa hapa milioni 204/- kwa ajili ya ujenzi wa zahanati 23 ni fedha kidogo sana.

Je, Serikali itakuwa tayari kuongeza fedha zahanati hizi 23 ziwezek kukamilika kwa wakati huu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka tuweke kwenye rekodi vizuri hapa. Mchungaji huyu pamoja na watu wake wamefanya kazi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba hii sera ya kujenga Zahanati katika ila kijiji. Kilichotokea kule Mbeya wame-over *mobilize*, yaani mwitikio umekuwa mkubwa mpaka unaona tatizo hili linalojitokeza hapa, ndicho anachokisema Mchungaji Mwanjale.

Kwa hiyo anachosema mtandaa wa panya huu ni ile mbao inayopita juu ya lenta na pale wanazo Zahanati 23 ambazo hazijakamilika. Ukitaka umsaidie huyu amalize zahanati amalize hizi zahanati 23 unahitaji 1.3 bilioni ambazo wao wameziomba humu kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hiyo. Lakini wakati huohuo wakaomba trekta lipatikane pale kwao kwa ajili ya kusomba takataka kule mjini. Likapitishwa trekta, hii haikupitishwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tuliwatengea milioni 191.6/- zimepelekwa zote zimekwenda. Mwaka huu tumewatengea milioni 204/- ni matumaini yetu zote zitakwenda pale. Katika hizi anazozisema hapa MMAM hii ambayo tumewatengea mwaka huu tumewatengea bilioni 1.2/- zitakwenda kule kwa ajili ya kwenda kufanya hiyo kazi.

Sasa liko swalii tunauliuza hapa, ninyi mlikuwa mnatenga bilioni 20/- sasa mnatenga bilioni 3/-. Ni kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti ndilo jibu lake. Lakini jitihada za Mchungaji na wenzake ni kubwa nataka nimpongeze tutakwenda kuliangalia jambo hili vizuri ili tusaidie hizi jitihada za wananchi zinazoendelea pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hii milioni 204/- anayosema kwamba ni kidogo, ndizo zilizopatikana na ndizo zilizopitishwa hapa.

Kwa hiyo, sasa ni suala la Mchungaji uende kule mka-rearrange priorities zenu. Mimi nikijibu hapa kwa niaba ya Waziri Mkuu nikasema tutawaongezeeni nyingine atakwenda kuniuliza kwamba wewe uliwaambia utawaongeza, ziko wapi?

Kwa hiyo, hii ni hali halisi na huu ni mfumo mzima wa bajeti lakini napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mchungaji pamoja na wananchi kwa kazi kuwa wanayoifanya pale.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na ya kujiamini sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ni ukweli kwamba Zahanati nyingi nchini hata zile ambazo zimekamilika bado hazina dawa na bado hazina wataalam wa kutosha.

Juzi nilikuwa Mbeya na kule lleje kuna Zahanati moja imekamilika ya kijiji cha Shinji naamini hali hiyo iko katika Zahanati nyingi Mbeya na nchini kote kwa ujumla. Waziri anatuambiaje kuhusu dawa na wataalam katika Zahanati ambazo zimekamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika ni kweli anachosema Mheshimiwa Zambi, ni kweli lakini pia anataka kujua jitihada gani zinazofanyika hapa. Waziri wa Afya amekuwa na jibu na sisi TAMISEMI tumekuwa tukijibu hapa.

Moja ya jambo ambalo tumefanya ni kuhakikisha kwamba *MSD* ihame kule iliko tukaipeleka katika kanda na tukasema dawa hizi zianze kupatikana hukohuko kwenye badala ya kwenda mpaka Dar es Salaam.

Pili pakaanzishwa mfumo unoitwa integrated logistic system uende ukabaini aina ya magonjwa yaliyoko maeneo mbalimbali.

Watu walioko Pwani wanamatatizo yao yanawasumbua, watu walioko kwenye maziwa wanamatatizo yanayowasumbua, walioko kule Kaskazini wanamatatizo yanawasumbua; wakabaini haya matatizo ili dawa zinazokwenda kule zifanane na aina na matatizo yaliyoko kule kwa sababu tulikuwa tunapeleka katika Zahanati nyingi zinakwenda zinamwagwa kwa sababu hazina *relevance* yoyote kwa matatizo yaliyopo pale.

Sasa anachokizungumza hapa tume-*address* nini? Tulichokifanya cha kwanza tumesema kwamba huu Mfuko wa Bima ya Afya tuhakikisha kwamba watu wanaingia katika utaratibu huu sio ule wa tele kwa tele au ule wa papo kwa papo.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba anachosema Mheshimiwa Zambi ni kweli. Lakini tukisimama imara ninayo *sample*, *sample* moja ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ambayo wameingia katika mfumo huu wa tele kwa tele wamepata pale milioni 250/- tukawapa milioni 250 nyingine wana milioni 500/- kwa mwaka uliopita. Hata siku moja Rombo hawakuwahi kusema wanatatizo la dawa katika eneo lao.

Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Zambi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, hebu twendeni tukawa-mobile wananchi wetu wajijunge na Mfukowa Bima ya Afya, wasipojunga katika hili jambo bado kelele hii itaendelea kupigwa hapa.

Lakini napenda nikiri kwamba kuna matatizo hayo na tutachukua hatua kuhakikisha kwamba dawa hizi zinakwenda kwa utaratibu huu uliosema.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kupata nafasi. Kama walivyosema Wabunge wengine suala hili la ujenzi wa Zahanati ni muitiko mkubwa kwa nchi nzima na jinsi ambavyo tunavyozungumza wananchi wanaendelea kujenga.

Je, Kwanini Serikali isitoe tamko na kuweka utaratibu kwamba angalau kila Wilaya iruhusiwe kiasi fulani cha Zahanati ili tupunguze tatizo hili na kuongeza ari ya wananchi kujitolea katika mambo muhimu kwa taifa letu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba arudie.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shekifu, hata mimi kidogo sikuelewa, naomba kidogo urudie.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba tatizo la ujenzi wa Zahanati ni tatizo la nchi nzima na ilikuwa ni maelekezo ya Serikali kwamba wananchi wajenge mpaka kufikia hatua ya mtambaa panya.

Wananchi wamefanya hivyo. Kwanini Serikali haitoi tamko ili ikiwezekana na kama imeshindika kuzisaidia Zahanati kila Wilaya iambiwe imetengewa kiasi gani ili zile ambazo zimeanza zijengeke na tulitoe tatizo hili kutoka kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nilikuwa sijampata kama ambavyo wewe hukumpata. Sera inasema hivi weka Zahanati katika kila kijiji na kama kuna vijiji viko karibukaribu weka mahali pa katikati waweze kusheria hiyo Zahanati.

Pili weka kituo cha afya katika kila kata, halafu weka hospitali ya Wilaya halafu weka hospitali ya Mkao ambayo inakuwa kama Hospitali ya Rufaa ndiyo mpango wenyewe huo.

Sasa Mheshimiwa Shikifu anasema kwamba kama hivyo ndivyo na kama inaonekana hela ni kidogo tutenge hela hizo zifulikane katika kila Halmashauri na tuweze kujua kwamba ni Zahanati ngapi zitajengwa katika hilo eneo. Ni wazo zuri katika jambo hilo lakini tutakuwa tunarudi nyuma.

Sisi tunachotaka kufanya hapa ni kusukuma Maendeleo kuhakikisha kila Kata inapata kituo cha Afya na Zahanati inapatikana katika kile kijiji. Sasa hii kutaja huwa tunaitaja kwa njia ya Bajeti.

Kwa hiyo, Bajeti mule ndani inaonyesha kabisa katika Bajeti utaona MMAM, MMAM ndiyo inahusika na masuala yote. Huu ni Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi ndiyo inayozungumza habari ya Zahanati na ujenzi wote unaofanyika kule. Ile nyagine ya *Basket Fund* ile inakwenda kwa ajili ya matibabu vifaa tiba na vidonge na vitu vingine.

Sasa hapo ndipo tumekuwa tumetamka kwamba kiasi hicho kimetengwa, kwa hiyo na Halmashauri itakwenda kujenga Zahanati zinazolingana na kiasi hicho kilichopatikana.

Lakini katika hili, tusiache jambo moja tunalolifanya toka tupate uhuru. Ule utaratibu wa wananchi wenyewe kusimama katika kutetea maendeleo na kufanya juhudhi kwa nguzu zao wenyewe huu moyo lazima tuendelee kuukuza katika Halmahauri zetu ili tuweze kufikia hatua ambayo tumetegemea kwamba tutafika.

7 JUNI, 2013

Na. 359

### **Ujenzi wa Barabara za Lami Kwenye Mji wa Kibaha**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. SILVESTRY F. KOKA) aliuliza:-**

Mji wa Kibaha ambao ni makao makuu ya Mkoa wa Pwani una Kilomita 1.5 tu ya barabara za lami licha ya ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga angalau kilomita 10 za lami mjini katika kipindi chake cha uongozi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya kwa Matiasi Msangani yenyeye urefu wa kilomita 10 na barabara za Kibaha Mjini Kilomita 5.40. ili kutekeleza ahadi hiyo ya Mhehsimiwa Rais tayari usanifu umefanyika na kukamilika kwa gharama ya shilingi milioni 90/- katika bajeti ya mwaka 2011/2012 Serikali imetumia shilingi milioni 716.9/- kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 1.135/-.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, Serikali imetua shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa barabara za lami katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Zabuni zimefunguliwa tarehe 3 Aprili, 2013 ili kumpata mkandarasi wa ujenzi.

Aidha katika mwaka wa fedha 2013/2014 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 1.2/- kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mji wa Kibaha. Hivyo, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa kwa kiwango cha lami kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini inavyoonekana ujenzi huu unakwenda taratibu sana. Napenda kujua pamoja na barabara hizi je, barabara ya kutoka Kibaha kutokea Baobab kupitia Vikawe kwa Madabida ujenzi wake umefikia wapi kwa maana kwa sasa umesimama na barabara ile imeharibi?

Mheshimiwa Spika, la pili barabara ya kutoka Kipatimu Milangalaya hadi Nyamwage ambayo wewe mwenyewe Naibu Waziri uliitembelea mpaka sasa pesa maalum ambazo tumeomba hatujapata majibu kwamba pesa hizo tutazipata lini?

**SPIKA:** Barabara ni za Pwani au za kwako huko? Kama ni za kwako hilo ni swali jingine kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza katika Mji wa Kibaha kulinagana na swali la msingi lilitsema kwamba lina kilomita 1.5 ni kwamba Mji wa Kibaha hauna kilomita 1.5 kwa sababu kwenye barabara iliyojengwa pale kutoka stand kwenda kwa Mkuu wa Mkoa hadi *TANESCO* ina kilomita 1.5 ambayo imejengwa na *TANROADS*kwa zaidi ya shillingi milioni 850/- lakini kutoka kwenye *junction* ile kwenye *TANZAM* Highway inayopita katika Mji wa Kibaha ni kilomita sita. Lakini kuna barabara nyiningine ya *TAMCO* kwenda Hospitali ya Tumbi kwenda Picha ya Ndege ambayo ina kilomita 4.5 nayo ni ya kiwango cha lami.

Lakini kingine ambacho napenda niseme katika Mji wa Kibaha katika Halmashauri ya Mji pamoja na Manispaa zinatakiwa zitumie vizuri fedha zinazopangwa pale kwa ajili

ya Barabara. Katika bajeti ya mwaka jana ambapo zilitengwa fedha nyingi kwa ajili ya kutumia hadi mwezi Machi katika milioni 475 walitumia milioni 114 tu ambayo ni asilimia 24. Hii ni Halmashauri ya Mji wa Kibaha. *Kibaha District Council* katika milioni 200 walizopewa walitimia milioni 92 tu. Lakini hata katiba bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 *District Council*/walibakiza milioni 75/- na Manispaa ya Kibaha wamebakiza pia fedha zaidi ya milioni 114.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wito wangu wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambapo Mbunge Koka anatoka aisimamie vizuri ili fedha hizi ziweze kutumika vizuri katika kutengeneza barabara pamoja na barabara zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika barabara zilizotajwa na Mhehsimiwa Mangungu tutazungumza na Waziri anayehusika na TAMISEMI kuangalia ni kwa namna gani tunaweza tukatumia fedha za Mfuko wa Barabara katika kuzitengeneza barabara hizo, kwa sababu katika Mfuko wa Barabara mwaka huu zimeongezeka fedha na zitakuwa zaidi ya bilioni 150 na hivyo zinaweza zikatumika kutengeneza barabara hizo. (*Makof*)

**SPIKA:** Haya tuendelee na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Mhehsimiwa Jaku Hashim Ayoub atauliza swali hilo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kuniona asubuhi hii ingawa mara nyingi umekiwa ukinisahau ikiwemo hata jana katika kuchangia Wizara ya Fedha sikupata bahati hiyo ingawa jina lilikuwa mbele ya kiti chako. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Sawa, lakini utaratibu haukuruhusu, wewe ulikuwa haujafikiwa.

7 JUNI, 2013

Na. 360

### **Huduma ya Maji Chuo Kikuu Morogoro (MUM)**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Chuo Kikuu cha Morogoro (*MUM*) kinakabiliwa na tazito la maji hali inayohatarisha afya za wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika katika chuo hicho?

(b) Je, ni hatua gani za haraka zitachukuliwa ili kuepusha majanga ya milipuko ya magonjwa kutokana na ukosefu wa maji chuoni hapo?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa (BLW), lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja na kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Morogoro, ni chuo binafsi ambacho hakinufaiki na ruzuku au fedha za Maendeleo za Serikali. Kwa mantiki hii, Chuo hutegemea sana vyanzo vyake vya ndani kuimarisha miundombinu yake ikiwemo upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, Chuo kina vyanzo viwili vya maji ambavyo ni maji yanayotolewa na Manispaa ya Morogoro ambayo kwa kiasi kikubwa hayatoshelezi matumizi ya wanachuo. Kwa kuzingatia changamoto hii, chuo kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato kilichimba visima viwili virefu ambapo cha kwanza kilijengwa mwaka 2008 na cha pili mwaka 2010. Kwa sasa hakuna uhaba wa maji isipokuwa tazito hilo linatokea kama kuna kukatika kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Milenia la Marekani (*MCC*) inatekeleza mradi wa ukarabati wa machujo ya maji ya Mambogo na Mafiga na ukarabati wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Morogoro. Mradi huu unatarajiwa kukamilika hapo mwezi Septemba, 2013 ambao utaongeza huduma ya maji katika maeneo ya Manispaa ya Morogoro ikiwemo Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM).

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana yaliyokidhi swali la msingi alilojibu Naibu Waziri muda huu naomba kumwuuliza swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni sababu gani za msingi zinazopelekea Chuo hicho hakipewi ruzuku, wakati Serikali imekuwa ikitoa karibu shillingi billioni 150 kila mwaka Iksaldia hospitali na Vyuo vingine.

Je, ni lini chuo hicho kitanufaika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali haitoi ruzuku kwenye vyuo vyote vya binafsi, viwe vya mashirika ya dini au watu binafsi na pengine pote. Tunachokifanya ni kwamba wale wanafunzi kwa sababu ni Watanzania, tunatoa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wote katika Vyuo vya Serikali na Vyuo Binafsi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru sana Naibu Waziri. Ni kweli labda kwamba hiki chuo ni chuo binafsi na Serikali haina mkono mkubwa lakini kwa kuwa pale pana mkusanyiko wa Watanzania wengi wanafunzi na suala la maji ni suala la maisha.

Je, haoni sasa basi angalau kwa sababu ya huo ubinadamu na kuwa wapo Watanzania wengi, Wizara inapaswa kupeleka angalau jenereta moja kama umeme utakatika ili waweze kupata maji?

7 JUNI, 2013

**SPIKA:** Kwa Wizara ya Elimu, haya Naibu Waziri naomba ujibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua kwamba Vyuo Binafsi na Vyuo vya Serikali wanaosoma pale ni watoto wetu Watanzania wote kwa pamoja kama zilivyo shule za msingi na sekondari *private na government*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia mradi ambaao upo pale Manispaa Morogoro kwa sababu ule mradi ni wa Serikali, lakini nimesema kwamba maji yatafika mpaka chuoni. Hata hivyo, bado chuo kina jenereta ambapo kipindi kingine huwa wanatumia jenereta ili waweze kupata maji pale.

Kwa hiyo ndiyo maana nimesema mpaka sasa tatizo la maji limekwisha, na baada ya huu mradi ambaao utachukua karibuni dola za Kimarekani milioni 8 ambaao unakwenda Manispaa ya Morogoro, ukiisha na ni mradi wa fedha za Serikali bado maji yatapatikana pale Chuo cha Morogoro.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika ahsante. Pamoja na kwamba ni Chuo Binafsi, lakini Je, Serikali haionti sasa badala ya kuona suala la kusomesha ambalo ni jukumu la Serikali, mashirika ya dini yanapokuwa yanafanya majukumu ya Serikali, ni wakati muafaka sasa wa kuelekeza nguvu ili kutatua tatizo ambalo kimsingi Serikali ni mzigo mkubwa ambaao inaelemewa, kwa hiyo itoe msaada mkubwa kwa Mashirika ya Dini ambayo yanasaidia *actually* jukumu la Serikali?

**SPIKA:** Umeelewa swali? Haya Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Msigwa unachokiongea hapa. Tunaposema Vyuo Binafsi, kwanza Serikali ndiyo inayoweza kutoa lthibati ili vile Vyuo vianzishwe.

Kwa hiyo, moja kwa moja ni kwamba Serikali inatambua kwamba Mashirika ya Dini yanapotaka kuanzisha mipango ya elimu, maana yake tunatambua kwamba wapo pale. Ndiyo maana nikasema hata hao wanafunzi wanaokwenda pale, wote wanachaguliwa na taasisi ya *TCU* na wanaokwenda pale ni watoto wetu wote wakifika pale wanakopeshwa na Bodi ya mikopo ambayo ndiyo Serikali yenewe.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema kwamba tunajaribu kuvizvezesha Vyuo hivi ili na vyenyewe viweze kuendeshwa kwa kuwakopesha wale wanafunzi ili Vyuo Vikuu vile vipate ada, hata pale Iringa kwako pana Chuo cha Tumaini, wale wanafunzi tunawakopesha na kile chuo ndiyo maana kinaendeshwa. (*Makofi*)

Na. 361

### **Kujenga Chuo cha VETA Mkoani Kagera**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera ni mionganini mwa Mikoa ambayo haina Chuo cha Ufundii:-

Je, Serikali itajenga lini Chuo cha Ufundii Mkoani Kagera kwa kuwa kuna sera ya kujenga Vyuo hivyo kila Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuwa na Chuo cha Ufundii Stadi katika kila Wilaya nchini, Serikali itajenga vyuo vipyaa au kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

7 JUNI, 2013

(*Folk Development Collages FDCs*) kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi ya Wilaya. Aidha, katika kutekeleza mpango huo, kipaumbele kinatolewa kwa kuanza na zile Wilaya ambazo hazina Vyuo vya ufundi stadi binafsi au Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera kuna Chuo cha Ufundi Stadi kinachomilikiwa *VETA* kilichopo Rwanishenyi, Bukoba Mjini. Aidha kuna Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika Wilaya za Misenyi (*Gera FDC*) kilichopo katika Jimbo la Nkenge, pia katika Jimbo la Biharamulo kuna chuo cha Rubondo *FDC*.

Vilevile viro vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi ambavyo ni Bwoki *VTC* na Kashasha *Village Technology Centre* vilivyopo katika Jimbo la Nkenge. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kuwashawishi wananchi na vijana wa Mkoa wa Kagera kuendelea kutumia Vyuo vya Ufundi Stadi vilivyopo kupata mafunzo wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kujenga vyuo vipyta.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Serikali wa kujenga vyuo vipyta, Wilaya za Chato na Misenyi zimefanyiwa utambuzi tayari wa stadi zitakazofundishwa na zipo katika awamu ya kwanza ya ujenzi.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri lakini naomba kusema kwamba Chuo jina kipo lakini Chuo maana yake ni kwamba kuna zana za kufundishia, kuna walimu, kuna vitendea kazi na kuna sura ya kuonesha kwamba hiki ni chuo. Kwa kweli chuo alichokitaja cha Bukoba siyo chuo sana ni chuo jina.

Ninaomba kuuliza ni lini, maana Wabunge wa Kagera tulikubaliana kwamba tunataka tujengewe chuo kama cha Chang'ombe katika Jimbo la Nkenge ambapo kuna nafasi ya kutosha, lini Serikali itatujengea chuo hicho.

Swali langu la pili, Naibu Waziri ametaja vyuo hivyo vitatu, vinne alivyovitaja lakini naomba anieleze, Serikali imesaidia nini katika Vyuo vile na lini mmekwenda kuvikagua kuona kama vinakidhi haja ya kuitwa Vyuo na kutoa watoto wanaoweza kupata elimu ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa anachosema Mbunge kwamba Serikali imekubali kujenga Chuo Wilayani Misenyi, na tunasema kwamba pale Gera tayari pamepatikana eneo ambapo tunasema kwamba kwa awamu ya kwanza katika hizi Wilaya 29 tutajenga chuo cha Wilaya pale Gera ambapo tayari Mbunge tumewasiliana kwamba pana uwanja wa kujenga chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, suala la pili juu ya vifaa vya hivi Vyuo ambavyo nlmevitaja baadhi ya Vyuo siyo vya Serikali na baadhi ya Vyuo hapa ni vya Serikali lakini vinamilikiwa na Wizara ya Mama Sophia Simba, ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na tunashirikiana kwa pamoja tuweze kuona kwamba kuna mapungufu gani ya vifaa ili tuweze kusaidia.

**SPIKA:** Hiyo Wizara ni ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na siyo Wizara ya Mama Sophia. Mheshimiwa Bura akifuaati na Mheshimiwa Laizer.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Wilaya ya Kongwa ni kati ya Wilaya kongwe nchini na kwa kuwa Wilaya hiyo haina Chuo cha Ufundi cha VETA na kidato cha Sita ni shule moja tu.

Kwa hiyo vijana wanaomaliza shule hawana pa kwenda kutokana na ukosefu wa kuwa na chuo cha Ufundi kwa ajili ya kujifunza ufundi.

Je, Waziri anaweza kunihakikisha kwamba Wilaya ya Kongwa ni kati ya Wilaya ambazo zipo katika mkakati wa kujengewa chuo cha ufundi?

7 JUNI, 2013

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Kongwa haipo kwenye *list* namba moja katika zile Wilaya 28 za kujengewa VETA kwa wakati huu, lakini Wilaya ya Kongwa ipo kwenye *list* namba Nne katika awamu ya.....

**SPIKA:** Mazungumzo wakati wa Bunge. Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kongwa itajengewa Chuo cha VETA katika awamu ya pili na ipo namba Nne. Kwa hiyo tutakapopata fedha najua tutajenga hivi vyuo vyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Laizer swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, hii awamu ya kwanza Naibu Waziri alitangaza, tangu aanze kuwa Naibu Waziri mpaka sasa anasema awamu ya kwanza na vyuo ni vilevile.

Je, ni lini Serikali itaanza hii awamu ya kwanza ili awamu ya pili nayo iweze kuendelea?(*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pengine ni ya kwanza katika ya pili. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba toka tumekuja hapa tunasema tutajenga Vyuo vya Wilaya na awamu ya kwanza tayari tulishapanga Wilaya 28, awamu ya pili Wilaya 15 na awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa ni namna gani tunavyoweza kupata fedha ili tuanze kujenga. Mwaka jana tulipata fedha na hata katika hotuba ya Waziri juzi hapa alisema kwamba tayari tulishaanza awamu ya kwanza. Tulipata fedha kidogo

tukajenga chuo cha Makete kimekwisha na mwaka huu kimeshaanza kuchukua tayari wanafunzi. Awamu hii tumeanza na Vyuo vitano, Wilaya ya Ludewa, Wilaya ya Kilindi, Ukerewe, Namtumbo na Chunya. Tayari kama nilivyosema kwamba viwanja vimeshapatikana na fedha kidogo zimeshaanza kuenda huko kwa ajili ya *feasibility study*, itakayofuata sasa ni katika Wilaya 29 tukipata fedha tunaendelea kuchukua ile list tumalizie moja kwa moja.

Taarifa njema ni kwamba Serikali imesaini makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB* ambapo kiasi cha dola za Kimarekani milioni 27 sawa na bilioni kama 43.2 tayari tumeposta tutaendelea kuanza kujenga hivi Vyuo vya Wilaya kadri ya tunavyoweza kwenda pamoja.

**SPIKA:** Maswali mafupi na majibu mafupi yanatoa nafasi kwa wengi, Mheshimiwa Lembeli kwa sababu nillikutaja sina namna.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Wilaya ya Kahama ni Wilaya pekee hapa nchini yenyе migodi miwili mikubwa ya dhahabu. Wilaya hii haina chuo cha *VETA*, kwa hiyo watumishi wengi katika migodi hii wanatoka Wilaya zingine na kuwaacha wananchi wa Kahama kuwa watazamaji.

Je, kwa utaratibu huu, na kwa sababu Kahama haipo katika *list* ya Wilaya zitakazojengewa vyuo vya *VETA*, kwa utaratibu huu, Serikali ni kweli inawatendea haki wananchi wa Wilaya ya Kahama? (*Makof*)

**SPIKA:** Naomba ujibu kwa kifupi pia tafadhali, maana yake ni chuo tu, haki au nini ni suala lingine lakini chuo tu ndio la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika *list* ya kwanza Wilaya ya Kahama haipo, lakini watalaam wetu walitembea nchi nzima kuweza kufanya utafiti wa kujua wapi pana chuo pana chuo cha *FDC* na wapi hapana chuo kabisa hata kama ni chuo

cha kanisa, ili mradi kama kinatoa mafunzo ya elimu ya Ufundu Stadi. Kwa hiyo, nadhani pale Shinyanga Kahama ni lazima patakuwepo na chuo hata kama ni cha binafsi. Kwa hiyo, kama pana chuo tusingeweza kuweka chuo kingine maana yake tunasema kwamba hizi Wilaya 29 hakuna chuo chochote hata kama ni chuo binafsi, chuo cha shirika la dini ama chuo cha Serikali, kwa mfumo wa chuo chochote maana yake kulikuwa hakuna kabisa ndiyo maana tulianza hizo Wilaya. Lakini kama nilivyo sema ni kwamba tumeshaanza kupata fedha tutaendelea, tukimaliza huko tutafika mpaka huko shinyanga. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, wale wanaofanya kampeni naomba wakae katika nafasi zao kwa sababu tunawafahamu, hawana sababu ya kupita pita.

Mheshimiwa Jafo rudi kwenye nafasi yako maana yake ni mwanzo wa fujo. (*Kicheko*)

Na. 362.

### **Uandaaji wa Mitaala ya Elimu**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. MOSES J. MACHALI)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani na kuhakikisha kuwa mitaala haiandaliwi na Taasisi ya Elimu Tanzania na badala yake iandaliwe na Mikoa au Wilaya ili kulinda na kuhifadhi mambo muhimu ya Kiutamaduni yanayoachwa katika mitaala ya elimu ya sasa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania (*TET*) ilianzishwa chini ya sheria Na. 13 ya mwaka 1975 ya Bunge lako Tukufu. Taasisi hii ni ya kitaalam inayoshughulikia mitaala ya elimu katika ngazi za elimu ya awali, ngazi ya elimu ya msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada.

Mheshimiwa Spika, aidha, mitaala ya Vyuo Vikuu husimamiwa na Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*) na mitaala ya Vyuo vya Elimu ya Juu visivyokuwa Vyuo Vikuu husimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*).

Mheshimiwa Spika, mitaala ya elimu na mafunzo huandaliwa na husimamiwa kitaifa ili kuweza kudhibiti ubora na hivyo kujenga umoja wa Kitaifa, sababu kuu ya kuwa na mtaala wa kitaifa ni kuweza kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa na kuwesha vijana wetu kuhimili ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa vile eneo la mitaala ni nyeti na lina uhusiano wa moja kwa moja wa maadili na sura ya Taifa kiuchumi, Kisiasa na Kiutamaduni, haitakuwa busara kuichia Mikoa na Wilaya kujitungia mitaala yake. Hali hiyo, inaweza kuathiri ubora wa elimu utolewayo Kitaifa na kusababisha matatizo katika mfumo mzima wa usimamiaji, uratibu, utahini na utoaji wa elimu bora kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mitaala yetu kuandaliwa kitaifa, upo unyumbulifu (*flexibility*). Unyumbulifu huo wa kuhusisha masuala ya kiutamaduni ya maeneo mbalimbali katika utoaji wa elimu. Dhana hii ya kitalaam inatoa fursa kwa mwalimu kuingiza maarifa yanayohitajika katika sehemu husika na kutumia rasilimali zilizopo katika mazingira ya ujifunzaji.

Aidha, walimu wameelekezwa kupitia mafunzo yao kutumia mifano na shughuli zinazotokana na mazingira ya wanafunzi. (*Makofii*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa hoja ya swali la msingi ni kuhusu mitaala na matatizo yanayotokea ni kwamba, baada ya Sera ni Mtaala, lakini kabla ya Mitaala tunatakiwa tuwe na *National Curriculum Development Framework*; na kwa kuwa nchi yetu haina *National Curriculum Development Framework* na kwa sasa tunaandaa Sera Mpya ya Elimu:-

- (i) Serikali haioni kwamba ni busara kuanza na *National Curriculum Development Framework* ili kuondoa utata kwa sababu amesema inategemea mazingira ya Kitanzania kama alivyosema lakini jiografia kwa shule sekondari *case study za human geography* zinafanyika za Nigeria?
- (ii) Kwa kuwa Mitaala hii inayozungumziwa; Taasisi ya Elimu, Baraza la Mitihani, Wizara husika, BAKITA, haviratibu kwa pamoja ili kuweza kutahini watoto wetu waweze kuwa na Taifa lenye mfumo wa kimaadili hasa udugu na utu wa mwanadamu, iweze kuwa ni elimu bora kwa Taifa letu. Je, Sera inayokuja itazingatia mambo haya muhimu ili Taifa letu liondokane na migogoro iliyopo sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Mstari ule wa nyuma, Mheshimiwa Turky na wenzako, mko Bungeni. Mheshimiwa endelea!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbatia, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbatia atakumbuka wiki mbili tu zilizopita, tulikuwa pamoja Wabunge wote na yeye alikuwepo, walipokuja Wataalam wa Wizara yetu kwa ajili ya kutoa Semina juu ya Rasimu mpya ya Sera ya Elimu. Mle ndani kuna mambo mengi sana na Mheshimiwa Mbatia yote ambayo ameyazungumza hapa yapo kwenye Rasimu ya Sera mpya, ambayo najua mpaka mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumeshaikimbiza tuweze kufanikiwa.

7 JUNI, 2013

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, tunazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbatia na mambo mengi ambayo yalikuwa kidogo yanaleta matatizo kwenye mitaala, vitabu, yako kwenye Sera mpya. Nadhani tumezingatia na mambo yatakwenda vizuri.

Na. 363

### **Kupeleka Umeme Mang'ola na Mbulumbulu**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY (K.n.y. MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE)** aliuliza:-

Serikali ilishatoa tathmini ya awali ya gharama ya kupeleka umeme Mang'ola kiasi cha Tsh.1.1 bilioni na tathmini ya kupeleka umeme Mbulumbulu kupitia Mradi wa REA pia ilishafanyika:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme Mang'ula ili kuwawezesha Wananchi wanufaikie na kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Eyasi?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kule Mbulumbulu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini, itatekeleza Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Mang'ola na Mbulumbulu ikihusisha vijiji vyote vitakavyopitiwa na Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, zabuni kwa kazi hizi zilikwisha tangazwa na sasa uchambuzi wa kupata mkandarasi wa

kutekeleza Miradi hiyo unaendelea kukamilishwa ili kazi hii ianze kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ghamara za kutekeleza Miradi yote katika Wilaya ya Karatu zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4.2 na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 1,217.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya wanakijiji wanaopata umeme huu mimi nashukuru.

(i) Wanakijiji wanataka kujua je, fedha hizi ambazo zimepangiwa Miradi hii hazipangiwi kazi zingine, yaani ni *ring fenced* ili wasije wakapewa tamaa baadaye wakakosa umeme?

(ii) Kwa muda mrefu sasa Miradi hii imekwama au imechelewa kwa sababu ya kupewa majibu kwamba hakuna nguzo au hakuna nyaya. Je, haya madai ni ya kweli; na kama ni ya kweli Serikali inachukua tahadhari gani? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mustapha Akunaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunawaunganisha Wananchi wengi kadiri tunavyoweza na ndiyo maana Serikali kuitia Waziri wa Nishati na Madini, ilitangaza hapa Bungeni pungozo la bei za kuunganisha umeme kwa Wananchi hasa wa vijijini na hata wa mijini. Sasa kutohana na pungozo hilo, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la maombi ya watu kuunganishiwa umeme na tangu bei mpya ilipotangazwa mpaka sasa, tumeshaunganisha watu wapatao 50,000.

Changamoto kubwa tuliyonayo ni kwenye nguzo na TANESCO imeshaagiza nguzo 65,000 na zinakuja awamu kwa awamu. Pia tunapata changamoto ya *logistic*, jinsi ya

kuzifikisha kwenye maeneo yaliyo mbali ili kuweza kuwaunganisha Wananchi wengi kwa wakati kama ambavyo wameomba.

Kuhusu suala la fedha, Miradi hii inapokuwa imetangazwa zile *tender* na kufunguliwa, fedha za *REA* hazitumiki kwa matumizi mengine yoyote bali zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa na Bunge.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na Serikali kujitahidi kuondoa tatizo la nguzo, lakini *TANESCO* bado wamekuwa na tatizo la kutokwenda kuondoa nguzo ambazo zimeanguka mahali. Kwa mfano, hivi sasa kuna nguzo zimeanguka Geita, *TANESCO* wamepigiwa simu hawajafika mpaka sasa. Hivi ni mpaka Waziri aende? Ahsante.

**SPIKA:** Haya. Kwa taarifa ulizopewa sasa hivi; Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni uzembe, kama *TANESCO* nguzo imedondoka tangu jana na wamepewa taarifa na hawajakwenda ku-*attend*, huo ni uzembe na hautakiwi kuvumiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kikao hiki, naomba nitoe agizo kwa Mameneja wa *TANESCO* Mkoa wa Geita na kote nchini, washughulikie matatizo haya haraka hasa nguzo zinapoanguka kwa sababu zinahatarisha usalama wa raia. Kwa hiyo, namwagiza Meneja wa *TANESCO* Geita ikifika saa sita mchana kama nguzo hiyo haijatoka basi nitachukua hatua. (*Makofii*)

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa

kuwa Serikali ilituwekeea umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo kupitia Mradi wa *REA*; na kwa kuwa katika tathmini yetu ya awali ulikuwa umeme huo ufike mpaka katika Hospitali ya Wilaya lakini nguzo zimeishia ndani ya kilomita moja ambapo umeme katika Hospitali ya Wilaya hakuna. Je, Serikali itakuwa tayari sasa *REA* watufikishie umeme katika Hospitali ya Wilaya ili Wananchi wapate huduma stahili katika Hospitali ile ya Wilaya?

**SPIKA:** Swali hili bwana ni jipya kabisa, tena zima zima. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, ambayo imepitishwa wiki mbili zilizopita, tulitoa maelezo hapa kwa kina kabisa kwenye Miradi yote ya *REA*. Popote ambako Mradi ule unapita; kuna hospitali, kuna shule, ni lazima zipewe kipaumbele na ziwekewe umeme. Kwa kutekeleza maagizo hayo, Wizara imezindua Mradi huu katika Wilaya ya Kongwa na shule zilizoko katika Wilaya ya Kongwa ambazo zimepitisha na Mradi zote zimepewa umeme pamoja na zahanati na vituo vya afya, visima ama pampu za kuvutia maji kwa Wananchi zote zilizoko pembezoni karibu na Mradi unakopita nazo zinapaswa kuwekewa umeme. Niseme tu kwamba, na wao wanapoandaa michoro ya ramani za kuptisha nguzo hizi, basi wazingatie kwamba sehemu kwenye vituo ama sehemu za visima au pampu za maji, wachore kwenye ramani yao na kuingiza katika Mradi, shule pamoja na zahanati. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, umeme huo utapelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo.

**SPIKA:** Ahsante, hiyo ndiyo *principal* inayotakiwa. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, atauliza swali hilo.

7 JUNI, 2013

Na. 364

## **Fedha kwa ajili ya Matengenezo ya Barabara ya Dodoma - Isangha hadi Igongo**

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Dodoma Mjini kupitia Chidilo, Changuluka – Chikopelo – Chali Makulu – Isangha hadi Chali Igongo iliyopandishwa hadhi kutoka Wilaya na kuwa Barabara ya Mkoa mwaka 2007/2008 na hali mbaya sana kiasi cha kutopitika wakati wa mvua; barabara hiyo inatengewa fedha kidogo sana kuliko hata ile iliyokuwa ikitolewa na Halmashauri ya Wilaya na hivyo kushindwa kufikia malengo ya kupanda daraja.

Je, ni lini barabara hiyo itatengewa fedha za kutosha ili iweze kutengenezwa na kuweza kupitika kwa wakati wote kwa ajili ya wakazi wa maeneo hayo?

**SPIKA:** Si fungeni mashine mnapokaa, maana tunasikia kila kitu, kuna wengine mashine zao zinawaka moto.

Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Barabara ya Chali Igongo hadi Chidilo Junction hadi Bihawana, ambayo inajulikana kama R. 433, yenye jumla ya urefu wa kilometra 68.77 ni Barabara ya Mkoa, inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROAD*) Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba, sehemu ya barabara hiyo kutoka Chidilo – Chinguluka – Chikopelo – Chali Makulu – Isangha hadi Chali Igongo

inapitika kwa shida hasa wakati wa masika, kutokana na ukweli kwamba sehemu ya barabara hii wakati inapandishwa hadhi, illikuwa pori na hivyo kuhitaji fedha nyingi kuifungua na kuifanya ipitike majira yote ya mwaka.

Mhesimiwa Spika, Serikali inaifungua barabara hii kwa awamu kila mwaka kadiri bajeti inavyoruhusu. Kwa mfano, kati ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 231.447 zilitengwa na kutumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya sehemu hii ya barabara. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, jumla shilingi milioni 576.873 zimetengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi na matengenezo ya muda maalum na matengenezo ya madaraja. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya matengenezo ya dharura na ujenzi wa daraja (*box culvert*) katika barabara hiyo.

Serikali itaendelea kuipa kipaumbele Barabara ya Chali Igongo – Chidilo – Bihawana, kwa kuifanya matengenezo makubwa kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha ili ipitike katika kipindi cha majira yote.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na shukurani ninazozitoa kwa niaba ya Wananchi wa Vijiji ambavyo vinapitiwa na barabara hiyo kwa matengenezo makubwa yanayoendelea katika barabara hiyo; nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa barabara hiyo sasa itapitika kiangazi chote lakini tatizo kubwa limebaki kupitika wakati wa masika kutokana na kutokuwepo kwa daraja kati ya Kijiji cha Chali Makulu na Chali Isangha. Je, Serikali sasa ipo tayari kutoa fedha na hasa hizi ambazo amezisema Mheshimiwa Waziri hivi punde kwamba zimeongezeka kwa mwaka wa fedha unaokuja kwa Wananchi wa vijiji hivi vinavyopitiwa na barabara hii ili daraja liweze kujengwa barabara ile ikamilike na iweze kupitika mwaka mzima?

(ii) Kwa kuwa Wilaya ya Bahi ina barabara moja tu iliyopandishwa hadhi tena hivi karibu ambayo tunaizungumzia hivi sasa hapa Bungeni; na kwa kuwa tayari tumeomba barabara mbili kwa miaka mitano iliyopita; Barabara moja ya kutoka Mzakwe – Lamaiti – Bahi na ya pili ya kutoka Chigongwe – Kigwe – Chikola na Chipanga: Je, Serikali ipo tayari pia kuzipandisha hadhi barabara hizo kwa ajili ya manufaa ya Wananchi wa Bahi?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omary Badwel, kama ifuatavyo:-

Kwanza, tunashukuru kwa pongezi zake alizozitoa kwa Serikali, kwa juhudini kubwa zinazofanywa katika kuifanya barabara hii ipitike. Aidha, amezungumzia kuhusu daraja ambalo anataka litengenezwe ili barabara hii iweze kupidika katika kipindi chote. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata katika bajeti ya mwaka huu, kuna fedha zingine zimeongezeka shilingi milioni 269 ambapo shilingi milioni 160 zitatumika kutengeneza barabara. Nina uhakika kutengeneza daraja hilo analolizungumzia ili barabara yote iweze kupidika katika kipindi chote cha mwaka.

Kuhusu maombi yake ya kupandishwa hadhi ya barabara; nataka niseme kwamba, hatuwezi kuchukua barabara zote zilizo chini ya Halmashauri za Wilaya; kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ilyoanzisha Mfuko wa Barabara, *percentage* fulani ya fedha huwa zinapelekwa *TANROAD* na *percentage* zingine huwa zinapelekwa Halmashauri za Wilaya. Katika bajeti ya mwaka huu, fedha zinazoenda kwenye Halmashauri za Wilaya zitafika zaidi ya shilingi bilioni 150.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba, asimamie vizuri hizo fedha zitakazopelekwa kwenye Halmashauri yake, zikatumike vizuri katika kutengeneza barabara zinazohusika na Halmashauri za Wilaya, kwa sababu kuna ushahidi wa kutosha kutoka Mfuko wa Barabara

kwamba, baadhi ya fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya katika kutengeneza barabara za Wilaya, hazitumiki vizuri na hivyo kuvunja Sheria ilioanzisha Mfuko wa Barabara, *Amendment Act No. 2* ya mwaka 1998 pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2006.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii.

**SPIKA:** Litakuwa la Bahi hilo swali; haya uliza.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Je, ni lini tena zoezi la kupandisha madaraja ya barabara litafanyika na Wizara ya Ujenzi kama ilivyofanyika mwaka 2010 kwani kuna barabara nyingi ambazo zinataka kupandishwa daraja lakini hili zoezi kama ilivyofanyika siku ile halijafanyika bado; kwa sababu kuna barabara kwa mfano Barabara ya Millola ...

**SPIKA:** Inatosha tu, ni lini zitatengenezwa na kupandishwa daraja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Je, ni lini zitatengenezwa? Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mikidadi, linalohusu kupandisha hadhi ya barabara kama ifuatavyo:-

Upandishaji wa barabara hadhi kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya kwenda kwenye *TANROAD* au kutoka *TANROAD* kwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya au kutoka *Regional Road* kwenda *Trunk Road*, unasimamiwa na Sheria Na. 13 ya mwaka 2007, katika Kifungu Na. 29. Kama nilivyojibu katika swali la msingi ni kwamba, hatuwezi tukapandisha hadhi barabara zote za Halmashauri za Wilaya. Jukumu ambalo tunalifanya sasa hivi kuititia fedha za Mfuko wa Barabara, tutahakikisha kwamba, fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya zinatumika ipasavyo kwa mujibu wa Sheria.

Tukifanya hivyo na Wakurugenzi wote na Wahandisi wote walioko kwenye Halmshauri zetu za Wilaya, wakasimamia vizuri zile fedha zinazopelekwa kule za Mfuko wa Barabara, ambapo kwa mwaka huu zimeongezeka zitafikia zaidi ya bilioni 150, patakuwa hakuna sababu ya Mbunge kwenda kuomba barabara yake ya Halmashauri ipandishwe hadhi ihamishiwe kwenye Wizara nydingine.

Kwa hiyo, wito wangu tuzisimamie Halmashauri zetu, fedha zote zinazopelekwa kule zitumike kwa makusudi yaliyokusudiwa kulinganana *Amendment Act No. 2* ya mwaka 1998 na mabadiliko yake ya mwaka 2006, ambayo yanasisitiza fedha zote zinazopelekwa kwenye barabara ni lazima zitumike kwenye Miradi ya Barabara tu. (*Makofii*)

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Wananchi wa Kilombero hadi Njombe, naomba swalii langu namba 365 lipate majibu. (*Kicheko*)

Na. 365

**Ujenzi wa Barabara ya Lami Toka Kidatu –  
Mlimba – Madeke**

**MHE. SUZAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Mkoa wa Morogoro ni kati ya Mikoa iliyoteuliwa kuwa Ghala la Chakula la Taifa na Wilaya ya Kilombero inazalisha kwa wingi sana mpunga na mazao mengine lakini hakuna barabara ya kuaminika kwa usafirishaji wa mazao hayo kwenda kwenye ghala na masoko:-

(a) Je, ni lini Barabara ya kutoka Kidatu – Mlimba hadi Madeke mpakani mwa Njombe itajengwa kwa lami ili kurahisisha usafirishaji wa mazao hayo?

(b) Kwa kigezo cha kupeleka barabara ya lami kwenye eneo lenye uwekezaji, Serikali haionti kuwa barabara hiyo imekidhi vigezo kwa sababu kuna uwekezaji mkubwa

wa kilimo cha mpunga unaofanywa na *KPL* kwenye Kata ya Mngeta?

**SPIKA:** Haya jirani; Mheshimiwa Waziri, ndio ujirani mwema huo unaitwa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sehemu hii ya barabara kutoka Kidatu – Ifakara – Taweta hadi Madeke, kiuchumi na kijamii, Serikali imekuwa ikijenga Barabara ya Kidatu – Ifakara, yenye urefu wa kilomita 73.2, kwa awamu kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Kati ya mwaka 2006 hadi 2008, jumla ya kilomita 16.17 zilijengwa kwa kiwango cha lami katika awamu mbili kuanzia Kiberege, yaani Magereza hadi Ziginali, kilomita kumi na kutoka Kibaoni Ifakara hadi Ifakara Mjini, kilomita 6.17. Aidha, Serikali imeshakamilisha kazi ya usanifu kutoka Kibaoni Ifakara hadi Ziginali, kilometra 16.8 Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kisha kuendelea kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kutohana na Mkoa wa Morogoro kuwa katika Ukanda wa Kusini wa Kilimo cha Tanzania (*Southern Agriculture Corridor of Tanzania – SAGCOT*), Serikali ya Marekani kuitia Shirika lake la Maendeleo la *USAID*, imekubali kugharamia kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara, kilometra 103.3, ambapo Mkataba wa Msaada wa Fedha (*Grant Agreement*), ulisainiwa kati ya Serikali na Shirika hilo, tarehe 23 Januari, 2013. Usanifu utakaofanywa ni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, utakaojumuisha pia upanuzi na ukarabati wa barabara na madaraja kwenye sehemu ya barabara ya lami kutoka Mikumi hadi Kidatu, kilometra 35.2 na hivi sasa taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Taweta – Madeke kwa kiwango cha lami, Serikali pia imepanga kuitekeleza kwa awamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa sehemu ya barabara ya kutoka Ifakara hadi Kihansi, kilometra 126. Awamu itakayofuatia ni kujenga sehemu hiyo ya barabara kwa kiwango cha lami, ili kuunganisha na kipande cha lami cha kilometra 24 kinachojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninapozungumza Kilombero mpaka Njombe, nina maana kwamba, Madeke ndiyo mpakani mwa Njombe na Kilombero na hii barabara ni muhimu sana.

(i) Katika majibu ya msingi ya Waziri, hiki kipande cha kutoka Mlimba mpaka Madeke Njombe, hajazungumza kama kitaanzia lini au upembuzi au changarawe ili tuweze kuungana na Wananchi wa Njombe katika kuinua uchumi. Je, ni lini sasa Serikali itaiwekea umuhimu barabara hii ili kufungua mipaka ya Wilaya hizi mbili?

(ii) Kwa kuwa unasema inaonekana kwamba Serikali imewekea umuhimu katika Wilaya ya Kilombero kwa kilimo cha *SAGCOT*; mimi nakubaliana na wewe lakini barabara muhimu hasa ninayoizungumzia ni kutoka Ifakara mpaka Mlimba, ambayo kwa kweli ukienda kule wakati wa mvua huwezi ukafika siku moja, unawenza ukalala njiani hata siku tatu. Je, ni lini sasa Serikali itatilia mkazo hii barabara ambapo Makao Makuu ya Wilaya na Hospitali yako Ifakara ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto kutohana na umbali na nauli kupanda na wawefe kupata mazao ya kutosha wawe na uchumi imara?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwa dhati kabisa kwamba, Serikali imeweka umuhimu katika kufungua maeneo haya. Na ndio maana kwa mwezi Januari, 2013 tumetiliana Mkataba na Serikali ya Marekani, ambapo barabara husika itafanyiwa *feasibility study* *detailed design* kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami. *Feasibility study* na *detailed design* zikatakapokamilika, ndipo tutajua ni wakati gani barabara hii tuta-*involve* kumwingiza Kandarasi kuweza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumhakikishia kwamba, katika bajeti ya fedha ya mwaka wa 2013/2014, Barabara ya Ifakara – Taweta – Madeke, imepangiwa jumla ya shilingi milioni 493 kwa matengenezo mbalimbali. Kwa hiyo, nina uhakika Barabara hii itaendelea kuitika, lakini pia na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa amependa kuyasemea ya kuweza kuunganisha mpaka katika Mkoa Mpya ambao wewe Mheshimiwa Spika, unakuhusu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, maeneo haya ni muhimu na Serikali inatambua hilo. Katika kutambua hilo pia, katika bajeti ya mwaka huu tumeanza kujenga Daraja la Kilombero, ambapo zaidi ya shilingi bilioni 53 zimetengwa pale na zimetolewa na Serikali kwa asilimia mia moja na Mkandarasi yuko kule kuhakikisha maeneo haya yote yanafunguka ili watani zangu kutoka maeneo hayo waweze kuja mjini vizuri kikamilifu. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa, ni Mteketa au nani? *Okay,* Mteketa!

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naitwa Dokta Haji Mponda.

**SPIKA:** Nilikuwa nashangaa kwa kweli ni Dokta Mponda, tafadhali.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nimekaa hapa mbele kwa sababu nikiaa kwenye nafasi yangu kule inakuwa vigumu kuniona. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mstari wa huko nyuma ni giza mara nyingi. Haya, Mheshimiwa Mponda!

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Serikali kwa kupitia Wafadhili, wametenga fedha kuanza kazi ya upembuzi yakinifu Barabara ya kuanzia Lupilo – Malinyi – Kilosa Mpepo – Londo – Lumecha hadi Namtumbo. Serikali ipo katika mchakato wa kumtafuta Mkandarasi, lakini ni muda mrefu sasa umepita.

Swali langu ni fupi tu kwa Mheshimiwa Waziri. Je, lini mchakato huu wa kumtafuta mkandarasi huyu wa upembuzi yakinifu wa barabara hiyo ya lami utaanza na sisi sasa Mkoa wa Morogoro moja kwa moja tukutane na Mkoa wa Ruvuma? Nakushukuru, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Barabara nyingine kabisa. Haya Mheshimiwa Waziri, maana wewe ni *computer* wa barabara, lakini swali jipya!

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Mponda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, katika bajeti ya mwaka huu ambayo ilipitishwa na Waheshimiwa Wabunge, tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kufanya *feasibility study* na *detailed design* inayounganisha Mkoa wa Morogoro hadi Mkoa wa Ruvuma kwa kiwango cha lami. Hatua hizo za kupitia nyaraka za kumpata *Consultant* aanze kufanya *feasibility study* na *detailed design* zinakamilishwa. Kwa vile ni wiki moja tu bajeti yangu imepitishwa na fedha ndiyo mmeidhinisha Bunge, nataka kumthibitishia

Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatua ya kumpata *Consultant* kwa ajili ya kufanya *feasibility study* na *detailed design* kwa barabara aliyoltaja, zitafanya kikamilifu ili kazi hizi ziweze kukamilika katika kipindi kifupi.

Na. 366

**Kuwawezesha Wanawake Kutumia Zana za  
Kisasa Katika Kilimo**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Moja ya sababu ya upungufu wa chakula nchini ni pamoja na Wananchi kutopenda kufanya kazi kwa bidii na maarifa hasa katika Sekta ya Kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mpya wa kuwafanya Wananchi wapende kufanya kazi kwa bidii na maarifa hasa katika Sekta ya Kilimo?

(b) Kwa kuwa idadi kubwa ya wakulima wadogo wadogo wanaotumia jembe la mkono ni wanawake na watoto wa kike. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inawawezesha wanawake ili waweze kutumia zana za kisasa?

(c) Je, ni wanawake wangapi wanamiliki zana za kisasa za kilimo nchini kama vile trekta na *power tiller*?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya vikwazo vinavyodumaza ukuaji wa kilimo ni harubu za kilimo cha mazowea, zinazowafanya baadhi ya watu na hasa vijana, kutopenda shughuli za kilimo. Njia moja ya kuwavutia Wananchi

kukipenda kilimo na kukiona kama ni ajira kama zilivyo ajira nyiningine ni kutumia zana za kilimo za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi iliyopita, asilimia 70 ya wakulima walikuwa wanatumia jembe la mkono, asilimia 20 walitumia wanyama kazi na hasa katika maeneo ya wafugaji kama Shinyanga na Mwanza na asilimia kumi tu ndio walitumia matrekta. Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, imeingiza nchini matrekta makubwa 9,148 na matrekta madogo, kwa maana ya *power tillers*, 5,520. Uingizaji huo umeleta mabadiliko ambapo hivi sasa wanaolima kwa jembe la mkono ni asilimia 62, yaani imepungua kutoka asilimia 70, wanaotumia wanyamakazi ni asilimia 24 na wanaotumia matrekta sasa ni asilimia 14.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wakulima, wakiwemo wanawake na vijana, Serikali imeweka utaratibu unaowawezesha kupata mikopo ya zana za kilimo yenye bei nafuu kuititia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, ambapo wakulima wanachangia asilimia 20 tu ya bei ya trekta. Aidha, mikopo yenye bei na riba ndogo inapatikana kuititia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na Dirisha la Kilimo kwenye Benki ya Maendeleo ya Taifa (*TIB*), iliyojulikana kama Benki ya Rasili mali. Mkakati mwengine ni huu wa sasa wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mikopo yote ya pembejeo na zana za kilimo haibagui jinsia. Hivyo, kwa sasa sina takwimu za wanawake wanaomiliki matrekta makubwa na matrekta madogo; hata hivyo, takwimu hizo zinaweza kupatikana baadaye. Aidha, natumia fursa hii, kuwahamasisha wanawake ama mmoja mmoja au katika vikundi vya uzalishaji na Wizara yangu itakuwa tayari kuwasaidia namna ya kupata zana za kilimo na pembejeo za kilimo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Benki ya *TIB* Makao Makuu yapo Dar es Salaam; na kwa kuwa Wanawake na Wananchi wengi wakulima wako vijijini; je, Serikali haioni umuhimu wa kufungua Dirisha la Benki hii katika kila Halmashauri ili Wanawake na Wananchi wengi waweze kunufaika na mikopo hii kwa sababu Serikali imedhamiria kuwandoa katika umaskini? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa Sensa ya Makazi na Watu ya mwaka 2012 katika dodoso lake ilitaka kujua ni Wananchi gani wanaomiliki zana za kisasa. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kutumia takwimu ya Sensa ya Wananchi ya Makazi kwa ajili ya kuwatambua Wanawake wote walio vijijini ili kuweza kuwawekea mazingira mazuri ya kuwasaidia kuwapatia pembejeo za kisasa za kilimo? Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili mazuri ya Mheshimiwa Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimeongea na Benki ya *TIB*, tena ni wiki mbili zilizopita, kuhusu mtandao wao katika nchi hii na wakanihakikisha kwamba, kwa utaratibu walionao, wao hivi sasa wanaweza wakawafikia wakulima popote pale nchini. Vilevile wapo katika utaratibu wa kuhakikisha kwamba, wanajitanua ili waweze kuwa na matawi katika maeneo yote katika nchi nzima. Kwa kweli, hili ni jambo zuri na wao wenyewe wako tayari na mimi nimezungumza nao.

Kuhusu hili suala la kutumia takwimu za sensa ni jambo zuri. Pia naomba nimwarifu Mheshimiwa Makilagi kwamba, sisi pia ndani ya Wizara, tumeanzisha utaratibu wa kuwa na Daftari la Wakulima. Daftari la Wakulima litakuwa linajua mkulima ni nani, yuko wapi, anafanya nini, analima hekta ngapi, zao gani na anapata huduma gani? Mfano mzuri kwa hivi sasa upo katika Mkoa wa Katavi, wao wamekwenda mbali zaidi; ukienda pale sasa hivi unaweza ukapata takwimu za kila mkulima na kile anachokifanya na tunataka utaratibu huu uwe *up-scaled* katika nchi nzima.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la utapiamlo ni kubwa sana nchini kwetu na hali ni mbaya sana kwenye maeneo makuu ya uzalishaji chakula katika nchi yetu.

Je, ni lini Serikali italeta kwa haraka Muswada unaoelekeza uwekaji wa virutubisho katika vyakula vitokanavyo na nafaka na mafuta?

**SPIKA:** Haya, pamoja na kwamba ni jipya sana, lakini zuri. Mheshimiwa Waziri, majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali zuri la Mheshimiwa Kitandula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, habari njema ni kwamba, siku hizi hatuzungumzii tu habari ya *food security*, tunazungumzia *food security and nutrition*; kwa hiyo, ni jambo ambalo Serikali inalizingatia. Suala la chakula bora, tumeliingiza katika Sera zetu za masuala ya usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na yeye kwamba, ipo haja sasa jambo hili kufahamika zaidi. Maana wengi sasa tunazungumzia usalama wa chakula, kwa maana ya kujitosheleza kwa chakula, lakini tunaingiza sasa *dimension* hiyo ya lishe katika chakula chetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe taarifa kwa Mheshimiwa huyu kwamba, kuhusu nafaka inawezekana wengi hawajajua; ipo aina nyingine ya mahindi ambayo kwa bahati nzuri mahindi hayo yanayo aina ya *protein*. Kwa maana kwamba, unaweza ukala mahindi hayo hayo peke yake kama ni uji au ugali, ukapata lishe na viini lishe ndani ya hayo mahindi. Nami nimewaaagiza wenzangu ndani ya Wizara, kuhakikisha kwamba, aina hii ya mahindi inaongezwa na inaweza ikatusaidia sana hasa katika maeneo kama ya Magereza na mashule, ambapo wanapata chakula cha

mkupuo kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa sababu anazo takwimu za sensa ana asilimia 62 ambayo bado haijaendelea; na kwa kuwa swali hili ambalo ameulizwa kifungu cha (b), kuwasaidia wanawake kutokana na matatizo kama haya: Je, ataweza kupata maendeleo gani kama hakutueleza mipango yake ya sensa na hii asilimia 62 kama ni Wanawake au ni akina nani?

**SPIKA:** Umeelewa swali hili? Mimi pia sikuelewa, hebu uliza kwa kifupi na halafu mashine hiyo ni kama haisikiki vizuri.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, asilimia 62 ambayo bado inatumia majembe ya mkono na ng'ombe buruta; na matokeo ya sensa na matokeo ya matrekta yote yaliyoletwa nchini; je, atatusaidiaje Waziri kutueleza Wanawake wamefaidika nini na suala hili la matrekta? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, asilimia 62 wengi ni Wanawake.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kama majibu yangu yatamtosheleza, lakini niseme hivi; sisi tunapotoa mikopo hii kwa kweli huwa hatuzingatii jinsia. Tunatoa mikopo kulingana na watu wanaokidhi matakwa ya wale wanaotoa mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ye ye kwamba, asilimia kubwa ya wakulima ni wanawake. Kwa hiyo, ipo haja ya kuangalia au hata wakati mwingine tuweke upendeleo maalum katika kutoa mikopo hii kwa ajili ya makundi haya. Nimelisema katika majibu yangu ya msingi kwamba, tutajitahidi kutafuta, kupembua kabisa kujua ni wakulima wa

kike wangapi wamepata mikopo ya aina hii na hatimaye tutafute njia ya kuweza kuwasaidia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tume-*relax* kwa sababu kazi zilizobaki ni chache.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Gosbert Blandes, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii kwamba, leo saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati ambacho kitakutana katika Ukumbi Namba 231.

Matangazo mengine; Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa Bunge (*TWPG*), Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie Wabunge Wanawake kuwa, kutakuwa na Semina kuanzia kesho tarehe 8 – 9 Juni, 2013, kwa siku mbili, kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote, iliyoandaliwa kwa pomoja kati ya Bunge la Tanzania na *CPA* Makao Makuu ya Uingereza katika Ukumbi wa Pius Msekwa, yaani *CPA* Tawi la Uingereza.

Lengo la Semina hii ni kuwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge, katika ushiriki bora wa masuala ya kisiasa pamoja na utungaji Sheria. Kwa hiyo, ujumbe wa Wabunge kutoka Uingereza, utajumuika nasi katika Semina hii kwa muda wa siku hizi mbili. Waheshimiwa Wabunge Wanawake, mnaombwa kuhudhuria Semina hii muhimu bila kukosa na Semina itaanza saa tatu asubuhi, tarehe 8. Aidha, leo tarehe 7, kutakuwa na chakula cha jioni saa moja kamili jioni katika Hoteli ya Dodoma (*New Dodoma Hotel*), kwa heshima ya ugeni wa Wabunge hawa; hivyo, Wabunge wote Wanawake mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, historia yetu sisi na Wabunge wa Uingereza, tulikuwa na utaratibu hata Wabunge wa kwetu wanakwenda kukaa Uingereza wiki mbili kwa Mbunge mmojawapo na sisi wenyewe kuja wanakaa huku kwetu kwa muda wa siku chache.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wanawake msikose hii semina, mnaweza kuwa na mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa wenzenu. Naomba sana maana yake mnaweza kukuta mpo mia moja na mnakwenda kumi. Kwa hiyo, mhudhurie ni muhimu sana sana.

Tangazo lingine ni kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa Mwenyekiti APNAC Tanzania, anaomba niwatangazie Wanachama wote wa APNAC kuwa leo tarehe saba kutakuwa na semina ya wanachama wote katika ukumbi wa *African Dreams Conference Centre* kuanzia saa saba mchana. Hawa ni wanachama wa APNAC, nadhani APNAC mnaifahamu.

Halafu Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumamosi tarehe 8 kwenye uwanja wa Jamhuri kutakuwa na michezo ya mpira wa miguu (*Football*) na mpira wa pete (*Netball*) kati ya Bunge *Sports Club* na timu ya Uhuru *Publication*.

Michezo hiyo itaanza saa kumi jioni, kesho asubuhi kutakuwa na mazoezi maalum ya viungo kwa wanamichezo wote katika uwanja wa Jamhuri, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa mazoezi na muziki, naona kutakuwa na mazoezi na muziki, ila mimi hapa sijaelewa.

Kwa hiyo, naomba pia mhudhurie jamani, mazoezi ni muhimu sana kwa afya zetu. Kama mnavyoona afya zetu kidogo zinatetereka bila utaratibu, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

### **Uchaguzi wa Wajumbe kwenye Taasisi na Vyuo vya Elimu ya Juu**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama tulivyotangaza awali tutakuwa na huu uchaguzi ambao tutashirikishwa kwa muda mfupi, kwa hiyo nitawasihi Wabunge wote mbakie mpaka tumalize kuchagua. Tukishamaliza kuchagua

mtakwenda kunywa chai, huko mnakokwenda kunywa chai, halafu mtarudi tena tutoe matangazo. Msipokuwepoo tutatangaza kwa redio.

Huyu Katibu ndiye Mkurugenzi wa kusimamia uchaguzi humu, Katibu.

**NDG. JOHN JOEL – KATIBU MEZANI:** Waheshimiwa Wabunge kama mlivyotangaziwa tarehe 27 Mei, 2013, leo ijumaa tarehe 7 Juni, 2013 na kama *order paper* inavyoonesha kutakuwa na uchaguzi wa wawakilishi katika Mabaraza ya Taasisi ya Elimu ya Juu nchini pamoja na jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika yaani *SADC Parliamentary Forum* ni kama ifuatavyo:-

Chuo Kikuu cha Dodoma nafasi moja; Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo nafasi moja; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya nafasi moja na Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika yaani, *SADC PF* nafasi moja.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi hadi kufikia muda wa mwisho wa kurudisha fomu hizo yaani Jumatano tarehe 5 Juni, 2013 saa kumi jioni wajumbe waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma ni Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, pamoja na Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ni Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni. Lakini leo asubuhi nimepokea barua ya kujitao Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu, kwa hiyo kwa nafasi hii Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni kwa mujibu wa utaratibu ambao Bunge hili Tukufu limejiwekea, mgombea wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni anapita bila kupingwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia aliyerudisha fomu ni Mheshimiwa Pindi Hazara

Chana, hakuwa na mgombea mwenza, kwa hiyo kwa mujibu wa utaratibu ambao Bunge hili Tukufu limejiwekea, mgombea wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya naye Mheshimiwa Pindi Chana anapita bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika yaani *SADC PF* waliorudisha fomu ni Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Leticia Mgeni Nyerere, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu na Mheshimiwa Lolesia Maselle Bukwimba, lakini jana jioni nilipokea barua ya Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu kujitoa. Kwa hiyo, nafasi hii wanaobakia kama wagombea na ambao wataoneshwa katika fomu ya kupigia kura ni Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mheshimiwa Leticia Mgeni Nyerere pamoja na Mheshimiwa Lolesia Maselle Bukwimba.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 8(2)(b) cha Nyongeza ya Pili za Kanuni ya Bunge kila mgombea kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika atatakiwa afike mbele ya wapiga kura yaani Waheshimiwa Wabunge ili kujieleza, kuulizwa maswali, kuyajibu na kuomba kura.

Baada ya kujieleza karatasi za kupiga kura zitatolewa ambapo kila Mheshimiwa Mbunge atatakiwa kupigia kura Mgombea mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo ya kwangu. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Huyu Mheshimiwa Leticia ni Mageni siyo Mgeni. Lughazitakazotumika Mheshimiwa Mkurugenzi?

**NDG. JOHN JOEL – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni zetu, hazikuweka utaratibu ulio wazi, lakini ningependekeza kwamba kwa jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika ingekuwa ni bora kikatumika Kiingereza. Nashauri tu kwamba, ingekuwa ni bora kikatumika Kiingereza kwa sababu huyu anatuwakilisha nje ya nchi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtu ana hoja anasimama.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi hii kwa kuweka heshima ya lugha yetu. Tunagombania kila siku kama tuheshimu lugha yetu ya Kiswahili ili ionekane ni kitu cha msingi. Sasa leo sisi ndio tunasema bora isemwe lugha hii, hapana, mimi natoa hoja.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kombo kwa sababu *AU* wametambua Kiswahili ni lugha ya Taifa na inatumika katika bara la Afrika na huu ni uchaguzi wa bara la Afrika, kwa hiyo ni vizuri Bunge letu likawa linatumia lugha yetu ya Kiswahili kuiendeleza. Leo tunatakiwa Walimu wetu kila mahali tuwapeleke kufundisha Kiswahili, sisi wenyewe tunarudi nyuma, haifai, tuenzi Kiswahili chetu. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati njema tuko Wabunge wanne hapa ambao ni wajumbe wa *SADC*, kule tunasema Kiingereza tu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu lugha ya kule ni ya Kiingereza, naomba tumhoji huyu mmoja kwa Kiingereza na mwagine huyu kwa Kiswahili. Kwa hiyo, nimeshafanya uamuzi tunahoji kwa Kiingereza kwa *SADC* tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mtulie kwenye viti vyenu, tunataka tuwahesabu na kengele ipigwe.

Waheshimiwa tutawapa hawa nafasi dakika tatu ya kujieleza, halafu mtawauliza maswali matatu kama yapo. Wagombea wote watoke nje tutawaita. Mtatakiwa kujieleza kwa dakika tatu na kama maswali yatakuwepo, yatakuwa matatu. Kwa hiyo wagombea wote wa vyuo vyote watoke nje maana siyo vingi.

Mheshimiwa Jafo tutawahesabu mara mbili, hebu mtoke nje wote, mtoke nje tutawahesabu mara mbili.

Naomba mtulie Mheshimiwa Lolesia, Mheshimiwa Leticia, Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe atoke nje kwa sababu tutawahoji wote, halafu tutapiga kura.

Naomba walioko nje waingie maana tunafanya kuhesabu sasa. Wagombea muwahesabu baadaye kwa sababu watakuja kupiga kura. Tunaweza kuanza.

